## HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA

### MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI CHA TAREHE 15/11/2021 KILICHOFANYIKA UKUMBI MDOGO KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Octavian Moshiro | - Afisa Kilimo na Ushirika (W) | - Mwenyekiti |
| 2. | Bw. Masoud Salum | -Afisa Ugavi (W) | - Katibu |
| 3. | Bi. Nyamayao Said | - Afisa Maendeleo ya Jamii (W) | -Mjumbe |
| 4. | Bw. Omari Kombo | -Afisa Elimu Sekondari (W) | - Mjumbe |
| 5. | Bw. Edwin Mwampamba | - Afisa Utumishi (W) | - Mjumbe |
| 6. | Bw. Erasto Msigwa | -Afisa Ufugaji Nyuki (W) | -Mjumbe |

WASIOHUDHULIA KWA TAARIFA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Bw.Patrick Mizimu | - Afisa Sheria | - Mshauri |

**MUHT.NA.01/01/2021-2022: KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alianza kwa kumshuru Mungu na kuwakaribisha wajumbe kisha alifungua kikao saa 6:34 Mchana

**MUHT.NA.02/01/2021-2022: KUPITISHA AJENDA ZA KIKAO**

Katibu aliwasilisha ajenda za kikao na wajumbe walizikubali kama ifuatavyo:-

1. Kufungua Kikao
2. Kupitisha ajenda za kikao
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha tarehe 30/06/2021
4. Taarifa ya manunuzi na utekelezaji kwa Robo ya kwanza ya Mwezi Julai hadi Septemba 2021
5. Kuidhinisha Njia ya “Single Source” katika miradi ya madarasa ya UVIKO-19 kwa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa na Serikali
6. Kuidhinisha Matumizi ya Force Account katika Ujenzi wa Miradi ya Maendeleo katika Halmashauri kwa Mwaka 2021/2022
7. Ununuzi wa POS za kukusanyia mapato
8. Taarifa ya mzunguko wa manunuzi (Circular Resolution)
9. Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti
10. Kufunga kikao

**MUHT.NA.03/01/2021-2022:KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA 30/06/2021**

Wajumbe walipitia muhtasari wa kikao cha tarehe 30/10/2021 na hapakuwa na masahihisho yoyote

| | |
|---|---|
| ................ | ........................ |
| KATIBU | MWENYEKITI |

**MUHT.NA.04/01/2021-2022: TAARIFA YA MANUNUZI NA UTEKELEZAJI KWA ROBO YA KWANZA YA MWEZI JULAI HADI SEPTEMBA 2021**

Taarifa ya manunuzi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa robo ya Kwanza ya Julai hadi Septemba 2021 iliwasilishwa. Taarifa ilionesha manunuzi katika Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mkinga, Ujenzi wa kazi za nje (Landscaping) na mfumo wa uvunaji wa maji ya mvua na tanki la maji la lita Milioni Moja katika jengo la Halmashauri. Manunuzi mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya ofisi ya Halmashauri kama dizeli, shajala na vinginevyo.
Taarifa ilionesha pia miradi mbalimbali ya maendeleo ya Halmashauri iliyotekelezwa kwa ''Force Account'' na za matumizi mengine katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga.
Baada ya mjadala wa kina wajumbe waliipokea na waliipitisha taarifa ya manunuzi na kuwa kumbukumbu sahihi.

**MUHT.NA.05/01/2021-2022: KUIDHINISHA NJIA YA "SINGLE SOURCE" KATIKA MIRADI YA MADARASA YA UVIKO-19 KWA KUZINGATIA MAELEKEZO YALIYOTOLEWA NA SERIKALI**

Katibu aliwasilisha barua yenye Kumb.CA.192/211/01/74 ya tarehe 12 Oktoba 2021 kutoka Mamlaka ya udhibiti wa ununuzi wa Umma (PPRA) yenye Kichwa cha habari **"utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye uzinduzi wa kampeni ya maendeleo kwa ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19".**
Wajumbe walipitia kwa kina barua hiyo na kujadili kwamba njia ya single source itumike kwa kuwa Ujenzi wa madarasa unatakiwa kukamilika haraka sana ndani ya Mwezi Disemba 2021 ili ifikapo Januari 2022 madarasa hayo yaanze kutumika. Kamati mbalimbali za utekelezaji wa miradi mashuleni ziundwe kwa mujibu wa mwongozo na zisimamie katika kuwapata wazabuni na mafundi wenye sifa, uwezo na uzoefu wa kufanya kazi na kwa kuzingatia thamani ya fedha kwa manunuzi yote yatakayofanyika.
Baada ya mjadala wa kina wajumbe waliridhia na kupitisha njia ya single source itumike katika kazi hizo na pia utaratibu utakaotumika ni wa Force Akaunti

**MUHT.NA.06/01/2021-2022: KUIDHINISHA MATUMIZI YA NJIA YA FORCE ACCOUNT KATIKA UJENZI WA MIRADI YA MAENDELEO**

Wajumbe walipitia na kujadili maelekezo ya Ujenzi na matumizi ya fedha kwa ajili ya Ujenzi wa Miradi ya Maendeleo inayotarajiwa kutekelezwa kwa Mwaka 2021/2022. Wajumbe walishauri kwamba ni vema taarifa mbalimbali kutoka katika ngazi za msingi (lower level) ziwasilishwe katkka bodi ya zabuni kabla na baada ya utekelezaji ili bodi iweze kujua na kushauri ipasavyo. Hivyo taarifa zinapowasilishwa Halmashauri kutoka ngazi za chini ni vema bodi ikapata taarifa mapema.

| | |
|---|---|
| ............... | ............... |
| KATIBU | MWENYEKITI |

Baada ya mjadala wa kina wajumbe walikubaliana kwamba matumizi ya njia ya Force Account yatumike katika Ujenzi wa majengo kadri maelekezo yatakapotolewa na serikali.

**MUHT.NA.07/01/2021-2022: UNUNUZI WA POS ZA KUKUSANYIA MAPATO**
Katibu aliwasilisha taarifa kwamba mawakala wa kukusanya mapato wanatakiwa kupewa POS kama ilivyoagizwa na Halmashauri na waheshimiwa madiwani. Hivyo baada ya mjadala wa kina wajumbe walipitisha ununuzi wa POS 48 kama ilivyoelekezwa kutoka kwa mzabuni M/S 5S GROUP LTD yenye jumla ya Tzs 27,904,262.40 pamoja na VAT. Mjumbe aliuliza kwamba inaonesha gharama ya POS moja ni shilingi 492,660/= bila VAT, Je Maelekezo ya Serikali gharama yake ni shilingi ngapi bila VAT? Katibu alisoma maelekezo ya Serikali na kwamba gharama ya POS moja haitakiwi kuzidi Tzs,500,000/= bila VAT.
Baada ya taarifa hiyo wajumbe walipitisha ununuzi wa POS hizo na kuwa kumbu kumbu sahihi ya kikao hicho

**MUHT.NA.08/01/2021-2022: TAARIFA YA MAAMUZI YA MZUNGUKO**
Katibu aliwasilisha taarifa ya maamuzi ya mzunguko kwa wajumbe wote kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Septemba 2021. Wajumbe walishauri ni vema taarifa hizo ziwasilishwe kwa wakati kama kuna uharaka. Baada ya taarifa hiyo wajumbe waliipokea na kuwa kumbu kumbu sahihi ya kikao hicho

**MUHT.NA. 09/01/2021-2022: MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI**
Mjumbe aliuliza kwamba malipo ya wajumbe wa bodi ya zabuni yamefikia wapi? Katibu alijibun kwamba tatizo lilikua kifungu ambapo mweka hazina alisema kiwekwe kifungu lakini dokezo lilishapitishwa. Wajumbe walikubaliana kifungu kitafutwe haraka na malipo yafanyike na pia maandalizi ya malipo yawe yanafanyika mapema kabla ya kikao kama tunavofanya katika vikao vingine vya kisheria.
Mjumbe alitaka kujua kiwango cha malipo kwa vikao vya bodi. Mwenyekiti alijibu kwamba wajumbe wanastahili kulipwa Tzs.150,000/= kwa kikao kwa mjumbe na pia mwenyekiti na katibu wanastahili kulipwa Tzs.200,000/= kwa kikao kwa mmoja.

**MUHT.NA. 10/01/2021-2022: KUFUNGA KIKAO**
Mwenyekiti alifunga Kikao mnamo saa 8:33 mchana

***UMETHIBITISHWA NA***

.........................
**KATIBU**

.........................
**MWENYEKITI**

**TAREHE:** 02/06/2022